BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

# BARAZA LA KUMI NA MOJA LA WAWAKILISHI

## MKUTANO WA TATU

**Kikao cha Kwanza – Tarehe 06 Mei, 2026**

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

Nakala zote za Gazeti Rasmi la Serikali pamoja na vijalizo vyake ambazo zimechapishwa kuanzia Mkutano wa Baraza uliopita kama ifuatavyo:

1. Toleo Namba 7439 la tarehe 30 Januari, 2026
2. Toleo Namba 7440 la tarehe 06 Februari, 2026
3. Toleo Namba 7441 la tarehe 06 Februari, 2026
4. Toleo Namba 7443 la tarehe 13 Februari, 2026
5. Toleo Namba 7449 la tarehe 13 Machi, 2026
6. Toleo Namba 7450 la tarehe 20 Machi, 2026
7. Toleo Namba 7453 la tarehe 02 Aprili, 2026
8. Toleo Namba 7454 la tarehe 02 Aprili, 2026
9. Toleo Namba 7455 la tarehe 02 Aprili, 2026
10. Toleo Namba 7457 la tarehe 02 Aprili, 2026
11. Toleo Namba 7458 la tarehe 02 Aprili, 2026
12. Toleo Namba 7459 la tarehe 02 Aprili, 2026
13. Toleo Namba 7460 la tarehe 02 Aprili, 2026
14. Toleo Namba 7461 la tarehe 10 Aprili, 2026
15. Toleo Namba 7464 la tarehe 24 Aprili, 2026

**Waziri wa Fedha na Mipango:**

Taarifa ya Serikali Kuhusu Mabadiliko ya Mafungu ya Bajeti kufuatia Muundo Mpya wa Serikali.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu Taarifa ya Serikali Kuhusu Mabadiliko ya Mafungu ya Bajeti kufuatia Muundo Mpya wa Serikali.

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi kwa mwaka 2026/2027.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi kwa Mwaka 2026/2027.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

302. MHESHIMIWA MOHAMMED ALI SALIM (Jimbo la Ziwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

    Kwa kuwa gharama za maisha zinazidi kupanda siku hadi siku, na kwa kuwa hali za Kaya Masikini zinazidi kuwa ngumu sana.

    Ni lini Serikali itafikiria kuongeza kima cha mafao ya kaya hizo masikini, ili kusaidia kupunguza ugumu wa maisha.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

77. MHESHIMIWA MAHFOUDH ABDALLA MOHAMMED (Jimbo la Magomeni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Naipongeza Serikali kwa kuhamasisha ujengaji wa madampo ya kisasa katika maeneo ya miradi ili kutunza mazingira.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga madampo (waste collection) hayo katika maeneo ya mradi wa mitaro ya maji machafu katika maeneo ya Magomeni Jitini, Kwamtumwajeni na Meya, ili kutunza mazingira katika maeneo hayo ya mradi.

**Wizara ya Kazi na Uwekezaji:**

59. MHESHIMIWA MOHAMMED MANZI HAJI (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Uwekezaji:

Kihistoria, Zanzibar ina utambulisho mkubwa wa ustaarabu wa Kiislamu, jambo ambalo linaweza kuwa fursa muhimu katika kuendeleza huduma na bidhaa zinazozingatia misingi ya Kiislamu, hususani katika sekta za fedha, biashara, utalii na huduma nyengine za kijamii na kiuchumi.

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kutoa motisha kwa taasisi na wawekezaji, ili kuanzisha na kuendeleza huduma na bidhaa zinazozingatia misingi ya Kiislamu.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuitumia fursa hiyo kama sehemu ya kukuza uchumi, uwekezaji na ajira kwa wananchi wa Zanzibar.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

120. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Pamoja na juhudi binafsi za viongozi wa Jimbo akiwemo Mwakilishi wa jimbo, bado kumekuwa na changamoto ya kupatikana maji matamu kwa wananchi wa Michamvi, hali ambayo ilikuwa mbaya zaidi katika kipindi cha mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

(a) Kwa kuwa kadhia hii imekuwa ya miaka mingi sana na wananchi wa Michamvi wameendelea kuwa na imani na

Serikali yao, ni lini utapatikana muarubaini wa kadhia ya ukosefu wa maji matamu kwa wananchi wa Michamvi.

(b) Kwa nini mamlaka yenye kusimamia suala hili (Rand Water), haifiki Michamvi kutoa ufumbuzi wa kadhia ya ukosefu wa maji matamu.

(c) Kwa kuwa wananchi wa Michamvi wamesubiri kupatiwa maji matamu tokea awamu zote za Serikali, je, katika Awamu hii ya Nane inayofanyakazi vizuri katika kuleta maendeleo, inawaahidi nini wananchi wa Michamvi katika kadhia yao hii.

409. MHESHIMIWA MARYAM SAID KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Kwa kuwa jimbo la Mkoani hususani katika vijiji vya Michenzani, Chokocho, Makombeni na Jondeni vinakabiliwa na changamoto kubwa ya upatikanaji wa maji safi na salama na kwakuwa tafiti zilizofanywa zimebaini kuwepo kwa vyanzo vya maji ya kutosha katika maeneo hayo na kwakuwa Serikali imenunua mitambo ya kisasa ya uchimbaji wa visima.

Je, Serikali ipo tayari kutoa mitambo hiyo kwa wananchi ili itumike katika kuchimba visima kwa lengo la kumaliza tatizo la maji katika eneo husika.

**<u>Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:</u>**

292. MHESHIMIWA ALLEY MASOUD ALLEY (Jimbo la Mtambile) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Kutokana na hali ya nyumba ya maendeleo iliyojengwa na Mzee Abeid Amani Karume iliyopo Kengeja kuwa mbovu sana, jambo linalohatarisha si tu maisha ya wakaazi wa nyumba hiyo bali na wapita njia.

Ni lini Serikali itaona umuhimu wa kulipatia ufumbuzi jengo hilo, ili kuwalinda wananchi na kuzuia janga linaloweza kuepukika.

**Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:**

339. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:

Kumeibuka hamasa kubwa kwa wananchi kujiunga na vikundi vya mazoezi, jambo linalochangia kupunguza maradhi yasiyoambukiza.

Je, Serikali imeweka mkakati gani wa kuimarisha miundombinu rafiki ya mazoezi, ili kuvisaidia vikundi hivi na kulinda afya za wananchi.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

452. MHESHIMIWA JUMA HASSAN THABIT (Jimbo la Fuoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Kihistoria, Zanzibar ni kisiwa ambacho miongoni mwa vyanzo vyake vikuu vya uchumi wake ni utalii na viungo (Spices) kama vile karafuu na viungo vyengine.

Je, ni upi mpango wa Serikali wa kuhakikisha kuwa na mazao mbadala yatakayouzwa nje ya nchi badala ya karafuu.

**Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:**

474. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:

Mifumo bila ya uhifadhi pamoja na ulinzi wake, ni jambo la hatari sana.

Je, Serikali imejipanga vipi na ina msimamo gani wa kuhakikisha mifumo yetu yote nchini ipo salama.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

316. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Sekta ya utalii imeendelea kukuwa na kuwa miongoni mwa sekta muhimu zinazochangia pato la taifa Zanzibar. Hata hivyo, ukuaji wa sekta hii haujaakisi ipasavyo katika kuimarisha ustawi wa kiuchumi wa wananchi wazawa hususani vijana na wajasiriamali wadogo.

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kuwa ukuaji wa sekta ya utalii unaongeza ushiriki na manufaa ya moja kwa moja kwa wananchi wazawa.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha vijana na wajasiriamali wadogo kupata ujuzi, mitaji na masoko ili waweze kushiriki kikamilifu na kunufaika na fursa zinazotokana na ukuaji wa sekta ya utalii.

(c) Je, Serikali imeweka utaratibu gani wa kuimarisha ushiriki wa wazawa katika uwekezaji na umiliki wa miradi ya utalii.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

262. MHESHIMIWA KHAMIS MOHAMMED AMRAN (Jimbo la Mkoani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Katika miaka ya hivi karibuni kumekuwa na tabia ya baadhi ya wakulima wasiokuwa wazalendo kuchoma moto mazao ili waweze kuyaingiza sokoni. Mazao hayo ni kama embe, ndizi na mapapai, jambo linaloharibu sifa na ubora wa vyakula na inaweza kupelekea madhara ya kiafya.

Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti jambo hilo.

**Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi:**

63. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Kwa nia nzuri Serikali imejenga kituo cha kupasisha gari na vyombo vya moto cha kisasa. Hata hivyo, kumekuwa na malalamiko kwa wamiliki wa vyombo vya moto kupata usumbufu. Malalamiko makubwa yamekuwa foleni, kufelishwa vyombo kwa kesi ndogo

zinazorekebishika na kutengenezwa mazingira ya kutoa fedha ili mtu apasishiwe chombo chake.

(a) Kutokana na malalamiko hayo ya wamiliki wa vyombo vya moto, ni lini Serikali itafanya uchunguzi binafsi wa kubaini ukweli wa malalamiko hayo na kuchukuwa hatua.

(b) Kwa kuwa kituo cha kupasisha gari ni kimoja kwa Unguja nzima na inachukuwa muda kupasisha vyombo vya moto kwa wakati, je, kuna mpango gani wa kujenga vituo vyengine kila Mkoa hapa Zanzibar, ili kuondosha adha ya foleni na kupoteza muda.

64. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Serikali inaweza kuokoa fedha nyingi za matibabu kwa kushajihisha wananchi kushiriki katika mazoezi yanayosaidia kulinda afya zao. Wananchi wengi wanashiriki mazoezi katika pwani ya Kizingo na wanatumia sana barabara inayoshukia pwani kutoka Kilimani Juu. Hata hivyo, barabara hiyo iliyowekwa kifusi imekuwa mbovu na kuchimbika.

Je, ni lini Wizara itachukuwa hatua za kuikarabati barabara hiyo, ili iweze kutumika vizuri na wananchi wanaotumia kushukia pwani ya Kizingo kwa shughuli mbalimbali, ikiwemo kufanya mazoezi ya kuimarisha afya zao.

<u>**Wizara ya Afya:**</u>

21. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Ni muda sasa tokea Waziri wa Afya mstaafu, Mhe. Nassor Ahmed Mazrui alipoahidi katika Baraza la Wawakilishi kwamba, Wizara yake itajenga Kituo cha Afya katika Kisiwa cha Kokota ambacho kina Skuli ya Msingi na Sekondari na wakaazi zaidi ya mia tatu, ambao hulazimika kutembea zaidi ya masaa matatu kuifikia Hospitali ya Wilaya ya Kinyasini.

(a) Je, ni lini Kituo cha Afya kitajengwa katika Kisiwa cha Kokota, ili wananchi wa eneo hilo wanufaike na huduma za kituo hicho.

(b) Kwa kuwa Serikali inafahamu kuwa kuchelewa kujengwa kwa Kituo hicho cha Afya ni kuzidi kuwaumiza wananchi hawa, ni ipi kauli ya Serikali ili wananchi wa eneo hilo

wajenge matumaini na Serikali yao.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

198. MHESHIMIWA MAHMOUD SHINENI ALI (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Ni miaka mingi sasa tangu Serikali ilipotangaza kupatikana kwa mafuta Zanzibar. Hata hivyo, hakuna taarifa yoyote iliyotolewa juu ya uchimbaji au hatua za kutumika kwa mafuta hayo.

(a) Kwa ajili ya maendeleo mapana na ustawi wa wananchi wetu, je Serikali imechukua hatua gani katika mpango wa kuanza kuchimba nishati hiyo ya mafuta yanayopatikana ndani ya Zanzibar.

(b) Kwanini Serikali haitoi taarifa rasmi kwa wananchi juu ya kukwama kwa uchimbaji huo.

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

68. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Kwa kuwa kwa kipindi kirefu kumekuwa na kilio cha mishahara midogo kwa watendaji wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, kilio ambacho kishazungumzwa sana katika chombo hiki, na kwa kuwa Wizara yako inaikumbuka ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wakati akiwaaga Wajumbe wa Baraza la Kumi la Wawakilishi, mwezi wa Juni 2025 kuhusu suala hili.

(a) Je, Wizara yako imefikia wapi katika kuhakikisha watumishi wa Baraza wanapata na kuimarishiwa maslahi yao hasa nyongeza ya mishahara.

(b) Kwa kuwa suala hili ni la muda mrefu sana na linazungumzwa kwa kila awamu ya Serikali, nini muarobaini wa kulimaliza ili watumishi hawa wasiachwe nyuma kimaslahi kama ilivyo watumishi wa mihilimi mengine.

(c) Tokea kutolewa kwa ahadi ya Rais kuwa amelipokea suala la maslahi ya watumishi wa Baraza, ni hatua gani zimefanyika kulitekeleza kwa kuwa Rais wetu ni muungwana na mwenye kutimiza ahadi zake.

## III. TAARIFA ZA SERIKALI:

Taarifa ya Serikali Kuhusu Mabadiliko ya Mafungu ya Bajeti kufuatia Muundo Mpya wa Serikali.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi kwa mwaka 2026/2027.

**Zanzibar,**
**06 Mei, 2026.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA LA**
**WAWAKILISHI, ZANZIBAR**